**1. MGODI ni nini?**

MGODI ni huduma ya kifedha inayowasaidia wateja wa Vodacom kuweka AKIBA na MIKOPO ya muda mrefu wa hadi siku 30. Huduma hii inatolewa kwa ushirikiano na benki ya Diamond Trust Bank (DTB).

**2. Nani Anastahili kutumia mkopo wa MGODI?**

Wateja wote wa Vodacom wanaotumia M-Pesa Zaidi ya miezi 6 wanaweza kutumia huduma ya MGODI na kufurahia huduma ya kuweka AKIBA na MIKOPO.
NB: Ustahili wa mikopo utategemea na kutofautiana kati ya mteja na mteja.

**3. Ni vipi mteja atajiunga na huduma ya MGODI?**

Piga *150*00#
Chagua 5 MIKOPO NA AKIBA
Chagua 3 "MGODI"
Chagua 1 "Ndio" kukubali vigezo na masharti
Weka Namba Ya Siri ya M-pesa
Utapokea ujumbe wa uthibitisho wa kujiunga na huduma ya Mgodi.

**4. Ni vipi mteja atapata mkopo kutoka MGODI?**

Piga *150*00#
Chagua 5 MIKOPO NA AKIBA
Chagua 3 "MGODI"
Chagua 1 "Mikopo"
Chagua 2 "Omba Mkopo"
Ingiza kiasi
Weka PIN ya M-Pesa
Utapokea ujumbe wa uthibitisho kuwa ombi lako limepokelewa na ujumbe wa SMS wenye taarifa za mkopo wako.

**5. Ni zipi gharama za mikopo ya MGODI?**

Mteja atalipia gharama ya 14% endapo akichukua mkopo wa siku 30 kutoka MGODI
Ikiwa mkopo utakaa kwa siku 30 bila kulipwa, adhabu ya 5% itaongezwa kwenye deni lake lililobaki.
Mteja anaweza kusogeza mbele muda wa kulipa deni lake na atalipia gharama ya 9% ya mkopo wake awali.

6. **Kwanini nichague kuongeza muda wa malipo ya mkopo wangu wa MGODI?**

MGODI inamruhusu mteja kusogeza mbele tarehe ya malipo ya mkopo wake kwa gharama ya 9% inayokatwa kutoka salio lake la M-Pesa.

Kufanya hivyo kunamuokoa mteja kupunguziwa kiwango chake cha kukopa kutoka MGODI.

7. **Jinsi ya kulipa mkopo wa MGODI**
   Piga *150*00#
   Chagua 5 MIKOPO NA AKIBA
   Chagua 2 “MGODI”
   Chagua 2 “Rejesha Mkopo”
   Chagua kama unataka “Kulipa Mkopo wote” au “Unataka Kulipa Kiasi Kingine”
   Ingiza kiasi
   Ingiza 1 Kuthibitisha
   Weka PIN ya M-Pesa

8. **Jinsi ya kuangalia kiwango cha mkopo unachostahili kukopa.**
   Piga *150*00#
   Chagua 5 MIKOPO NA AKIBA
   Chagua 3 “MGODI”
   Chagua 1 “Kiwango cha matumizi”

Utapokea ujumbe wenye taarifa za mkopo unaostahili kupata.

9. **How can a customer request for Outstanding Loan balance?**
   Piga *150*00#
   Chagua 5 MIKOPO NA AKIBA
   Chagua 3 “MGODI”
   Chagua 5 “Salio La Mkopo”
   Weka PIN ya M-Pesa

Mteja atapokea ujumbe wa SMS wenye taarifa ya deni lake la mkopo wa MGODI

**10. Je inawezekana kuchukua mkopo Zaidi ya mmoja kutoka MGODI?**
Hapana, kwa sasa huduma ya MGODI inakuruhusu kuchukua Mkopo mmoja tu na utaweza kuchukua mkopo mwengine pale ambapo mkopo wako wa mwanzo umelipwa kikamilifu.

11. **Nini kitatokea ikiwa nitakaa Zaidi ya siku 30 bila kulipa deni langu la MGODI?**
   Endapo utakaa na deni la MGODI bila kulipa kikamilifu kwa Zaidi ya siku 30, gharama ya kuvusha ya 5% itaongezeka kwenye deni lako lililobakia.

Na ifikapo siku ya 120 bila kukamilisha malipo, tutakuripoti kwa mamlaka za usimamizi wa Mikopo na Madeni, kitu ambacho kitakukosesha mkopo mwengine kutoka taasisi yoyote ya kifedha nchini Tanzania.

12. **Kiasi gani ninatakiwa kuweka Akiba kabla ya kustahili mkopo wa MGODI?**
Huhitaji kuweka Akiba yoyote ili upate mkopo wa MGODI. Ila kuweka akiba na MGODI kutakuongezea kiwango unachostahili kupata kama mkopo wa MGODI.

13. **Ni vipi naweza kuweka akiba na MGODI?**
Kuweka Akiba na MGODI fuata hatua zifuataz:

Piga *150*00#
Chagua 5 MIKOPO NA AKIBA
Chagua 2 "MGODI"
Chagua 2 "Akiba"
Chagua 1 "Weka Akiba na MGODI"
Chagua "Dunduliza" kuweka Akiba ya muda mfupi au "Akiba Ya Muda Mrefu" kuweka Akiba ya kuanzia miezi mitatu na Zaidi.

14. **Kuna mifumo mingapi ya kuweka Akiba na MGODI?**
Uwekaji wa Akiba kwenye huduma ya MGODI upo katika mifumo miwili:

a) Akiba ya muda mfupi (Dunduliza) – mfumo wa uwekaji akiba ya muda mfupi inayotoa rejesho la 3.75% kwa mwaka inayohesabiwa kila siku na kulipwa kwa mwezi.
b) Fixed Deposits – mfumo wa uwekaji akiba ya muda maalumu (miezi 3/6/au 12) ambao unampa mteja gawio/faida ya hadi 5.44% kutokana na kiwango cha akiba yake pamoja na muda wa akiba aliyoweka.

15. **Ni Faida/Gawio kiasi gani inayotolewa ukiweka akiba na MGODI?**

MGODI inatoa faida ifuatayo endapo mteja ataweka akiba.

| FIXED DEPOSIT | | | |
|---|---|---|---|
| Months | 1 – 500,000 | 500,001 – 1,000,000 | > 1,000,000 |
| | Buckets Amounts TZS | | |
| 3 | 3.94% | 4.13% | 4.31% |
| 6 | 4.50% | 4.69% | 4.88% |
| 12 | 5.06% | 5.25% | 5.44% |

| DUNDULIZA -NORMAL SAVINGS | |
|---|---|
| 1- 10 mil | 3.75% p.a calculated daily and paid monthly |

16. **Nini kitatokea endapo Akiba yangu itafika muda wake wa kulipwa?**

    Baada ya miezi 3/6/12 ya kuweka Akiba na MGODI, kiwango cha Akiba yako pamoja na faida vitawekwa kwenye akaunti yako ya akiba ya muda mfupi (Dunduliza) na utaweza kuitoa kwenda akaunti yako ya M-Pesa moja kwa moja.

17. **Nini kitatokea endapo nitafunga akaunti yangu ya Akiba ya Muda Mrefu kabla ya muda wake?**

    Endapo utafunga au kusitisha akaunti yako ya fixed Deposit kabla ya muda wake, kiwango cha akiba yako kitapelekwa kwenye akaunti yako ya Dunduliza na unaweza kuihamisha kwenda salio kuu la M-Pesa na kufanya miamala mingine.

    NB: Kufanya hivyo kutakukosesha faida/gawio ulilostahili kupata awali endapo ungeacha akaunti yako ya Akiba imalize muda wake.

18. **Nifanye nini ikiwa nina swali, maoni, au tatizo kwenye huduma ya MGODI?**

    Endapo unapata changamoto kuhusu huduma ya MGODI au unahitaji kutoa maoni au maswali kuhusu huduma hii, tufikie kwa kupitia chaneli zetu za huduma kwa wateja jwa kupiga namba 100, au kupitia kurasa zetu za kijamii, na kutembelea maduka yetu yanayopatikana nchi nzima.